**SEHEMU YA KWANZA :LUGHA** *Muda: Saa 1 Dakika 40*

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

**1.** Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 50.

**2.** Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-

*(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako*

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi hadi 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne.***

***Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Mara ____1____ kilipolia, wachezaji wa pande ____2____ mbili walijitokeza____3____ wakionekana____4____ huku ____5____ wanaringaringa. Watu wakawafanya waongeze____6____ yao kwa kuwashangilia kwa ____7____ na makofi na ____8____. Haukupita____9____ mrefu walitengana ____10____ sehemu zao na kipenga cha kuanzisha mchezo kikalia. Naam, timu zilianza____11____shika, mara____12____ ukatupwa huku na huko,kila upande____13____ kupata ushindi lakini ____14____ hizo ziliendelea hadi mwisho. Tulizidi kupiga moyo____15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** kengele | **B.** firimbi | **C.**kipanga | **D.**kipenga |
| **2.** | **A.**yote | **B.**kote | **C.**zote | **D.**wote |
| **3.** | **A.**uani | **B.**ugani | **C.**usanjani | **D.**uyogani |
| **4.** | **A.**wana shati | **B.**watumishi | **C.**mabanati | **D.**watanashati |
| **5.** | **A.**wakawa | **B.**wakikuwa | **C.**wakiwa | **D.**wawe |
| **6.** | **A.**madaha | **B.**madoa | **C.**mzaha | **D.**vipawa |
| **7.** | **A.**hoi | **B.**vigelegele | **C.**hoil hoi | **D.**vifujo |
| **8.** | **A.**mbija | **B.**bija | **C.**binja | **D.**mbinja |
| **9.** | **A.**mda | **B.**muda | **C.**kipindi | **D.**wasaa |
| **10.** | **A.**katika | **B.**kwa | **C.**ndani | **D.**kando |
| **11.** | **A.**vita | **B.**kufa | **C.**pata | **D.**vuta |
| **12.** | **A.**mpira | **B.**kandanda | **C.**kanda | **D.**mchezo |
| **13.** | **A.**ukiwania | **B.**ukitaka | **C.**wakitaka | **D.**ukionea |
| **14.** | **A.**vilio | **B.**mapambano | **C.**mvutano | **D.**kukurukakara |
| **15.** | **A.**ndondi | **B.** ngumi | **C.**konde | **D.**bao |

__*Kuanzia swali la 16-30, jibu swali kulingana na maagizo.*__

16. Malipo ya fedha anayopewa mtu aliyestaafu aghalabu kila mwezi ni.

A. koto B. pensheni
C. marupurupu D. fidia


17. Mtu anayetunza vitabu katika maktaba huitwa;

A. katibu B. mnajimu
C. mhazili D. mkutubi

18. ***Hana mbele wala nyuma*** ina maana kuwa:

A. Yeye ni bwanyenye
B. Yeye ni mlala heri
C. Maskini hohehahe
D. yeye anabahati sana

19. Sehemu **"z"** katika mchoro huu huitwa:




A. mche B. kigoda
C. mpini D. ankara

20. **Andika wingi wa:**
**Karatasi yangu ilipotea**

A. Karatasi yangu ilipotea
B. Makaratasi yetu yalipotea
C. Makaratasi zetu zilipotea
D. Karatasi zetu zilipotea

21. Mwindaji haramu wa wanyama ni:

A. jangili
B. msasi
C. jambazi
D. mporaji

22. Mwanamume ambaye hapati watoto huitwa:

A. tasa B. gumba
C. matege D. kibyongo

23. Ugonjwa unaosababishwa na mbung'oma kuleta usingizi ni ipi?

A. Malale B. Tauni
C. Kihcocho D. Kideri

24. ***Kijana alinguka tapwi !*** maana yake ni kuwa alianguka

A. sakafuni B. majini
C. matopeni D. mchangani

25. ***Andika kwa umoja***
Milango mikubwa ilitolewa na wezi

A. Mlango mnene ilitolewa na wezi
B. Mlango mkubwa ulitolewa na wezi
C. Kilango kikubwa kilitolewa na mwizi
D. Mlango mkubwa ulitolewa na mwizi

26. ***Andika tarakimu hizi kwa maneno***
***Elfu kumi na mbili, mia na mbili***

A. 12102 B. 120212
C. 1202 D. 121200

27. Kitenzi ***"lia"*** katika kauli ya kutendesha kitakuwa

A. lilisha B. liza
C. lisha D. liliza

28. Wino, uyoga, ugali na wali ni majina katika ngeli gani?

A. U - ZI B. I - ZI
C. U - U D. U - YA

29. Dawa za kulevya yaani ____ zinadhuru afya zetu kila tunapotumia

A. mihadharati B. mihambarashi
C. mihiramu D. mihadarati

30. Ni methali ipi isiyohimiza jitihada katika maisha?

A. Papo kwa papo kamba hukata jiwe
B. Achanikiaye mpinini hafi njaa
C. mstahimilivu hula mbivu
D. kofi haziliii ila kwa viganja viwili

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Twamshukuru Mwenyezi, kwawe mwingi ukarimu
Alo na kitu cha enzi;Mola wetu Akramu
Kutupa kitu azizi; lugha kuitakalamu
Lugha huwa ni kitamu, ujuapo kutumia.

Lugha mkuu mlezi, aleaye vinadamu
Hata wanyama ja mbuzi, wana lugha wafahamu
Hufungua simulizi, izaayo tabasamu
Lugha huwa ni kitamu ujuapo kutumia.

Lugha hodari mkwezi, akweaye tata ngumu
Huzifyeka pingamizi, zizushazo uhasimu
Likazidisha mapenzi, wapendanao kudumu
Lugha huwa ni kitamu, ujuapo kutumia

Lugha ndiyo mpagazi, mazito kuyahudumu
Pia hupanga vizazi, pasi mbari kudhulumu
Aidha hufanya kazi, ikwawa mustakimu
Lugha huwa ni kitamu, ujuapo kutumia

**31.** Kiini cha shairi hili ni
A. maombi B. kuzungumza
C. lugha D. ukarimu

**32.** Shairi hili lina beti ngapi
A. nne B. nane
C. mbili D. tatu

**33.** Kila ubeti una mishororo mingapi?
A. minne B. miwili
C. nne D. minane

**34.** Kina cha kati cha shairi hili ni
A. li B. zi
C. a D. sha

**35.** Chagua mshororo wa tatu wa ubeti wa tatu
A. aidha hufanya kazi, ikawa mustakimu
B. likazidisha mapenzi, wapendanao kudumu
C. hufungua simulii, izaayo tabasamu
D. kutupa kitu azizi, lugha kuitakalamu

**36.** Kila mshororo una mizani ngapi?
A. kumi na tisa
B. kumi na nne
C. sitini na nne
D. kumi na sita

**37.** Malenga anasema kuwa lugha ni kitu kitamu
A. watu wakiongea
B. ikiwa timamu
C. ukijua kuitumia
D. ikitumiwa na wataalamu

**38.** Kwa nini mtunzi anamshukuru Mwenyezi Mungu?
A. kwa kuketi kiti cha enzi
B. kwa kuwa mtu azizi
C. kwa kutupa lugha ambayo ni kitu kizuri
D. kwa kuwafanya watu wapendane

**39.** Ni kitu gani ambacho hakijatajwa kuwa ni chanzo cha lugha?
A. uhasama B. kuzungumza
C. kushirikiana D. upendo

**40.** Kiitikio cha shairi hili ni gani?
A. Twamshukuru Mwenyezi; kwawe mwingi ukarimu
B. Hata wanyama ja mbuzi, wana lugha wafahamu
C. Likazidisha mapenzi, wapendanao kudumu
D. Lugha huwa ni kitamu, ujuapo kutumia

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 41 - 50.***

Kutokana na uchovu uliojumuika na ubao, Jabari alijikuta akisinzia. Kwa kuwa mpiga mluzi huishia kuimba, hatimaye alilala. Akiwa usingizini, aliona mambo ya kutisha, zimwi lilitokea kwenye ukuta wa nyumba yake ya msonge na kumkaba koo. Alijaribu kupambana nalo lakini nguvu zake hazikufua dafu hata chembe!

Zimwi lile lilipokuwa likinuia kummeza mzimamzima ***kitungule*** alitokea mlangoni akidanadana na kuligota jichwa la zimwi lile kwa nguvu mno. Zimwi liliudhika na kughurika. Liliamua kumshika kitungule yule lilipokuwa limeshika kitungule mikononi. Jambo la kushtua lilitokea. ***Miale ya moto ilitoka kwenye shahada ya kitungule yule na kuyachoma macho ya zimwi.*** Ajabu nyingine ni kuwa miale ya moto ilikuwa miekundu kama damu.

Do! staajabu ya chawa uyaone ya kiroboto. Zimwi lilia kwa maumivu likaanguka chini na kufa. Alipokuwa katika hali ya kushangaa, kitungule akamwambia kuwa siku zote awe wa kutumia busara na hekima katika maisha. Kitungule yule alianza kudanadana na kwenda nje. Jabari alibaki kinywa wazi huku akiwa na maswali mengi kichwani. Katika kutaka kumwandama ndipo alipozinduka usingizini.

Alikuwa ametokwa na jasho akaloa chepechepe. Alipotupa macho kila upande, aliona kitungule akiwa pale pale nyasini. Aliamua kumjongea kwa nia ya kumwuliza yaliyotokea ndipo hali ikawa vile kwa ujasiri mkuu uliotangamana na tahadhari, alimkaribia kitungule kisha akachutama kando yake na kuuliza, "ulifikaje hapa?"

---

**41.** Ni kwa nini Jabari alisinzia?
A. machofu na mbao nyingi
B. uchovu na njaa
C. machofu na njaa
D. uchovu na kazi

**42.** Kwa mujibu wa aya ya kwanza, Jabari aliposinzia,
A. Alikuwa karibu kuuawa na zimwi
B. Alishambuliwa na zimwi
C. Alikabwa roho na zimwi
D. Alikumbwa na jinamizi

**43.** Kifungu ***"hazikufua dafu"*** hakina maana ya
A. kuota mleli
B. kuambulia patupu
C. kutoka mkono mtupu
D. kuambulia nunge

**44.** Kwa mujibu wa aya ya pili, kilichomwokoa Jabari ni
A. kitungule B. nguvu
C. jichwa D. zimwi

**45.** Miale ya moto iliyotokwa ilikuwa tamthili ya
A. ngeu B. urujuani
C. moto D. hariri

**46.** Maneno 'staajabu ya chawa uyaone ya kiroboto; yanachukuana na methali
A. Ajabu ya ngamia kucheka nundu ya ng'ombe
B. Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi
C. Asiye na wake ana Mungu
D. Ukistaajabu ya Musa utayona ya Firauni

**47.** Ni nasaha ipi murua aliyoipata jasiri kutoka kwa kitungule?
A. Atambue umuhimu wa hekima katika maisha yake
B. Aepukane na hekima na busara katika maisha yake
C. Awe mzoefu wa kutumia busara na hekima katika maamuzi yake
D. Asijihusishe na busara wala hekima katika maisha yake

**48.** Kwa mujibu wa kifungu, Jabari alizinduka usingizini
A. alipotaka kumwandama kitungule
B. kabla ya kitungule kumpa nasaha
C. baada ya kitungule kuliua zimwi
D. baada ya kitungule kwenda nje

**49.** Ni ajabu gani iliyomkumba Jabari alipozinduka kutoka usingizini
A. kitungule alikuwa pale pale nyasini
B. kitungule alitoweka na kuwamacha peke yake
C. Zimwi lilikuwa limeaga dunia baada ya kupigwa na kitungule
D. Kitungule kumpa mawaidha kuhusu maisha

**50.** Kifungu hiki kinaweza kupewa mada
A. Kitungule na zimwi
B. Jabari na kitungule
C. Mawaidha na kitungule
D. Ndoto ya Jabari.